**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAISI-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBAHA**

Mawasiliano,

Mkuu wa shule 0713033946.

Makamu mkuu wa shule 0686110816

SHULE YA SEKONDARI MAGINDU,

S.L.P 30118,

KIBAHA.

13/05/2024.

**KUMB.NA.MSS/J.5/2024/2025**

**MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI………………………………….**

**S.L.P………………..**

**YAH: KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KWA MWAKA WA MASOMO 2024/2025 KATIKA SHULE YA SEKONDARI MAGINDU.**

## 1. UTANGULIZI

Ninayofuraha kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kuendelea na elimu ya sekondari kidato cha tano katika shule hii kwa mwaka 2024/2025 na utasoma tahasusi ya……………. Muhula wa masomo utaanza tarehe …………. muda wa kuripoti ni kuanzia saa 7:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni, aje akiwa amevaa sare ya shule.

## 2. SHULE ILIPO

Shule ipo Mkoa wa Pwani,Halmashauri ya wilaya ya Kibaha, kata ya Magindu umbali wa kilomita 20 kutoka unaposhukia standi ya mji mdogo wa Chalinze.Usafiri wa kufika shuleni upo muda wote na unaweza kupanda pikipiki kwa shilingi 5000/= au gari kwa shilingi elfu 3000/=.

## 3. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

i. **MICHANGO YA SHULE**

Fedha zinazohusu michango ya shule zilipwe kwenye akaunti ya shule namba **21201200107** katika Banki ya **NMB**. (tafadhari andika jina la mwanafunzi kwenye banki payment slip).

ii. Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi/mlezi

Michango mbalimbali

| Na | Aina ya mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa uendeshaji wa shule | **65,000/=** |
| 2. | Tahadhari | **5,000/=** |
| 3. | Nembo | **5,000/=** |
| 4. | Kitambulisho cha shule | **5,000/=** |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

Shule haipokei fedha taslimu, fedha zote zilipwe kupitia banki ya **NMB** tawi lolote kwa kutumia namba za akaunti husika na stakabadhi ya malipo (banki payment slip) zenye jina kamili la mwanafunzi ziletwe shuleni siku ya kuripoti.Hakikisha unabaki na nakala ya karatasi ya banki(BPS)

## 4. SARE ZA SHULE

| WASICHANA | WAVULANA |
|---|---|
| i. Sketi mbili zenye urefu wa kufika vifundo za miguu rangi ya kitambaa ni daki bluu mshono ni rinda box<br>ii. Mashati meupe ya mikono mirefu mawili<br>iii. Soksi ndefu nyeupe jozi mbili au zaidi<br>iv. Sweta la rangi daki bluu yenye shingo ya V<br>v. Tai ya rangi ya daki bluu<br>vi. Viatu vyeusi vya kufunga na kamba<br>vii. Tsheti ya kola rangi ya kijivu yenye nembo ya shule<br>viii. Sketi mbili ya rangi damu yam zee(maluni) urefu kifundo cha miguu (rinda boksi)<br>ix. Traki suti ya rangi ya blue yenye mistari miyeupe pembeni isiwe ya kubana na fulana yake ya rangi hiyo hiyo yaani jezi yenye kola<br>x. Raba nyeupe ,viatu vya michezo ,bukta ya bluu na taiti ndefu nyeusi,<br>xi. Kandambili na vitenge pisi mbili<br>xii. Nguo ya kulalia rangi nyeupe (pajama) | i. Suruali mbili za rangi ya daki bluu pana zisiwe modo pamoja na turn up miguuni<br>ii. Mashati meupe ya mikono mirefu mawili<br>iii. Soksi ndefu nyeusi jozi mbili au zaidi<br>iv. Sweta la rangi daki bluu yenye shingo ya V<br>v. Tai ya rangi ya daki bluu<br>vi. Viatu vyeusi vya kufunga na kamba<br>vii. Tsheti ya kola rangi ya kijivu yenye nembo ya shule<br>viii. Suruali mbili ya rangi damu ya m zee(maluni) isiwe modo<br>ix. Traki suti ya rangi ya blue yenye mistari miyeupe pembeni isiwe ya kubana na fulana yake ya rangi hiyo hiyo yaani jezi yenye kola<br>x. Raba nyeupe ,viatu vya michezo ,bukta ya bluu<br>xi. Kandambili na taulo |

NB:Kwa wanaovaa hijabu watashona nusukanzu nyeupe (badala ya shati jeupe).
Nguo za nyumbani haziruhusiwi.

## 5. MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI

i. Bunda (rimu) za karatasi mbili kwa kila mwaka
ii. Shuka (4) za rangi ya bluu kwa wavulana na pinki kwa wasichana
iii. Ndoo moja ndogo,madumu mawili,kijiko,sahani ya bati ya vyumba,kikombe (1),chupa ya chai ndogo na chupa ya maji ya kunywa.
iv. Tochi ya betri kwa tahadhari ya umeme isiwe ya kuchaji
v. Madaftari makubwa (counter books) angalau 10
vi. Scientific calculator
vii. Kitambulisho cha bima ya afya kama unacho
viii. Godoro jipya futi mbili na nusu
ix. Chandarua mpya ya rangi ya blue kwa wavulana na nyeupe kwa wasichana
x. Flat file

6. **VIFAA VYA USAFI**
   i. Fagio la ndani lenye mpini mrefu(soft broom) 01
   ii. Reki 1,fagio la chelewa ndefu ya nje(fagio la wima)
   iii. Squeezer moja(mpira wa kukaushia maji)
   iv. Fyekeo moja
7. **MAMBO MENGINE MUHIMU KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.**
   a. Medical examination fomu ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali .Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara atakapo ripoti shuleni
   b. Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi kutoshiriki katika migomo,fujo,na makosa ya jinai.
   c. Fomu ya mzazi ya kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
   d. Kopi ya cheti cha kuzaliwa
   e. Kopi ya result slip
   f. Picha ndogo mbili(passport size)

Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA

**DISCIPLINE FOR SUCCESS**

**……………………**

**MOSES F.BAKARI**

**MKUU WA SHULE**

# SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

**I.** Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na **25** ya mwaka **1978** na kama ilivyorekebishwa kwa sheria **Na 10** ya mwaka **1995**.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na mafunzo yenye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya **RAIS TAMISEMI** lenye jukumu la usimamizi wa uebdeshaji Elimu . Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

i. Heshima kwa viongozi,wazazi /walezi,wafanyakazi wote,wafanyakazi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.Mahudhurio mazuri katika shughuli za ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shuleni.
ii. Kushiriki kwa umakini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
iii. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine atakazopewa
iv. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje mipaka hiyo wakati wa uwanafunzi wako katika shule hii.
v. Kutunza usafi wa mwili ,mavazi,na mazingira ya shule
vi. Kuvaa sare za shule wakati wote
vii. Kutunza mali za umma
viii. Kuzungatia ratiba ya shule wakati wote.

**II.** Makosa yafutayo yanaweza kusababisha kusimamishwa shule au kufukuzwa

i. Wizi
ii. Uasherati na Ushoga
iii. Ubakaji
iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine,mirungi,kuli n.k
v. Kuharibu makusudi mali za umma
vi. Kudharau bendera ya Taifa
vii. Kuoa au Kuolewa
viii. Kutoa mimba
ix. Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu
x. Kukataa adhabu kwa makusudi

# KIAMBATANISHO A

# FOMU YA HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili la mwanafunzi kama lilivyotumika katika mtihani wa kidato cha nne ……………………………………………………………………………………………

2. Tarehe ya kuzaliwa mwanafunzi:Tarehe…….…..,Mwezi……………,Mwaka…………
3. Mahali alipozaliwa mwanafunzi.
   i. Kijiji……………
   ii. Wilaya…………
   iii. Mkoa……………

4. Kabila la mwanafunzi…………………
5. Jinsi…………………………………….
6. Dini/dhehebu…………………………….....
7. Jina la Baba:……………………………
   Namba ya simu:………………………..

8. Jina la Mama:…………………………
   Namba ya simu:……………………….

9. Kama unalelewa na mlezi Jina kamili…………………………………..
   Uhusiano na mwanafunzi:……………………………………………..

10. Shule ya sekondari alikotoka mwanafunzi………………………………
11. Jina la Mwenyekiti wa serikali za Mtaa…………………………………
    Namba yake ya simu:……………………………

12. Je ana magonjwa sugu? Kama ndio taja……………………………………..
    Anatibiwa hospitali gani? ……………………………………………….

SAINI …………………  TAREHE ……………..

# KIAMBATANISHO B

# HALMASHAURI YA WILAYA KIBAHA.

**(ANUANI YA MZAZI)**

……………………………..

………………………………..

………………………………

**YAH: HATI YA KUKUBALI MASHARTI KUHUSU MTOTO WANGU KUSOMA SHULE YA SEKONDARI MAGINDU.**

Mimi……………………………………………….(jina la mzazi/mlezi wa mwanafunzi)
Mzazi/Mlezi wa……………………………………………………. Jina la mwanafunzi.

Aliyekuwa akisoma shule ya ………………………………………………( taja jina la shule aliyosoma mwanafunzi) Katika wilaya ya………………………….. Mkoa wa………………

Ninakubali mtoto wangu asome shule ya sekondari Magindu,iliyopo Halmashauri ya wilaya Kibaha na nitazingatia sheria ,kanuni na taratibu zote za shule kama zilivyoelekezwa katika fomu mbalimbali na kwamba;

A. Mtoto wangu atahudhuria masomo kama kawaida na kufanya shughuli zingine zote za shule akikaa shuleni kwa kipindi chote cha miaka miwili ya kidato cha tano hadi cha sita.

B. Kwa muda wa miaka miwili sitamsumbua Mkuu wa shule,Afisa elimu sekondari ,Wilaya na Mkoa kuomba uhamisho.

Sahihi ya mzazi/mlezi Tarehe

………………….. ……………

## SHULE YA SEKONDARI MAGINDU

## FOMU YA KIAPO CHA MWANAFUNZI KUTOSHIRIKI MIGOMO, FUJO PAMOJA NA MAKOSA YA JINAI

Mimi…………………………………………………………….Ninakubali nafasi niliyopewa katika shule ya Sekondari Magindu .Ninaahidi kuwa mtiifu na kufuata kikamilifu **SHERIA,KANUNI** na T**ARATIBU** halali zilizopo .Pia ninaahidi kufanya bidii na kushirikiana na uongozi wa shule na wanafunzi wenzangu katika kuendeleza taaluma na shughuli zingine nitakazopangiwa .Naahidi kutoshiriki katika migomo ,fujo na makosa ya jinai.

| **JINA LA MWANAFUNZI** | **SAHIHI** | **TAREHE** |
|---|---|---|
| ….………………………… | ………………… | ... …… |

**NAKALA**

1. Afisa Elimu Mkoa,
   S.L.P 30080,
   **PWANI.**

2. Mkurugenzi Mtendaji,
   Halmashauri ya Wilaya Kibaha,
   S.L.P 30153,
   **KIBAHA.**

3. Afisa Elimu Sekondari,
   Halmashuri ya Wilaya Kibaha,
   S.L.P 30153,
   **KIBAHA.**

4. Afisa Elimu Kata,
   Kata ya Magindu,
   S.L.P 30153,
   **KIBAHA.**

MAGINDU SECONDARY SCHOOL P.O.BOX 30118, KIBAHA,

STUDENT'S MEDICAL EXAMINATION FORM.

TO THE MEDICAL OFFICER IN CHARGE

………………………………………………..

……………………………………………….

……………………………………………..

Please, examine the under named student and note any medical complications towards her joining this school

STUDENT NAME………………………………..… AGE……… CLASS………..

1. Blood (any infection noted)…………………
2. Blood group…………………………………
3. Urine analysis (not pregnancy)………………………
4. Stool………………………………..
5. Ears (hearing strength)………………….
6. Chest………………………..
7. Abdomen…………………..
8. Heart diseases………………………….

Any chronic complaints which needs attention of the school authority

…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

Name of the medical officer……………………………………………………………………..

Designation……………………………………………………

Station ……………………………………………………………

Official stamp……………………………………………….

……………………

MOSES.F.BAKARI

HEAD MASTER